TRC
# Reli na Matukio
Desemba 18, 2018 Toleo Namba 10.





TRC imeongeza Huduma ya Usafiri wa Abiria kwa treni ya Deluxe mara mbili kwa wiki kutoka Dar es Salaam (Alhamis Saa 2 Asubuhi na Jumapili Saa 4 Asubuhi) na kutoka Kigoma (Ijumaa saa 2 Usiku na Jumatatu Saa 2 Usiku)

# TUMESIMIKA, TUNAZIDI KUSONGA MBELE

## HIZI NDIZO SIFA KUU ZA NGUZO ZA UMEME UTAKAOENDESHA TRENI ZA KISASA









Kazi ya Usimikaji wa Nguzo za Umeme utakaotumika Kuendesha treni za Kisasa zitakazotumia Umeme na Reli ya kisasa - SGR imeanza eneo la Soga nje Kidogo ya Kambi ya Ujenzi wa Reli ya Kisasa liyopo Soga mkoani Pwani mapema Desemba 2018.

Zifuatazo ni sifa za nguzo za Umeme zitakazoendesha treni za Kisasa:-

- Nguzo zinajengwa umbali wa Mita 50 kutoka nguzo moja hadi nyingine.
- Urefu wa nguzo moja ni Mita 9.5.
- Uzito wa nguzo Moja ukiwa Tani 2.4.
- Zina uwezo wa kudumu kwa kipindi ncha Miaka 120.
- Nguzo zimewekewa madini ya Zinki kwa ajili ya kuzuia kutu.

Ujenzi wa Reli ya Kisasa ni utekelezaji wa Ahadi za Serikali ya awamu ya Tano chini ya Rais Mhe. Dkt. John Pombe Magufuli.

## KAZI YA UKARABATI WA MABEHEWA YAENDELEA KWA KASI - TRC



Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano Mhandisi Isack Kamwelwe (wa pili kushoto) akikagua kazi ya ukarabati Mabehewa ya Mizigo na Abiria ikiwa ni utekelezaji wa ahadi ya serikali ya awamu ya tano chini ya Rais Dkt. John Pombe Magufuli kutoa fedha kwa ajili ya kukarabati mabehewa ili kuongeza tija na ufanisi wa Shirika katika kutoa huduma ya usafiri wa Abiria na Mizigo alipotembelea Karakana ya Shirika la Reli Tanzania jijini Dar es Salaam na kukuta mafundi wakiendelea na kazi ya kukarabati Mabehewa Desemba 2018.





Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano Mhe. Isack Kamwelwe akikata utepe kufungua awamu ya pili ya mafunzo yaliyoandaliwa na Shirika la Reli Tanzania kwa lengo la kuandaa wataalam watakaosimamia Shughuli za Uendeshaji wa reli ya kisasa - SGR pindi utakapokamilika ikiwemo uendeshaji treni za umeme, ukarabati wa reli ya kisasa pamoja na kusimamia mifumo mipya ya mawasiliano na umeme, mafunzo yanatolewa na wakufunzi kutoka nchini Uturuki katika ukumbi wa Kambi ya Ilala jijini Dar es Salaam hivi karibuni 2018.




Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Reli Tanzania Ndugu Masanja Kungu Kadogosa akizungumza wakati wa hafla ya ufunguzi wa awamu ya pili ya mafunzo maalum yaliyoandaliwa na Shirika la Reli Tanzania kwa lengo la kuandaa wataalam watakaosimamia Shughuli za Uendeshaji wa reli ya kisasa pindi utakapokamilika ikiwemo uendeshaji treni za umeme, ukarabati wa reli ya kisasa pamoja na kusimamia mifumo mipya ya mawasiliano na umeme, mafunzo yanatolewa na wakufunzi kutoka nchini Uturuki katika Ukumbi wa Kambi ya SGR Ilala jijini Dar es Salaam hivi karibuni 2018.




Washiriki wa Mafunzo, baadhi ya wafanyakazi wa TRC pamoja Waandishi wa Habari wakimsikiliza kwa makini Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Reli Tanzania Ndugu Masanja Kungu Kadogosa wakati wa hafla ya ufunguzi wa awamu ya pili ya mafunzo maalum yaliyoandaliwa na TRC kwa lengo la kuandaa wataalam watakaosimamia Shughuli za Uendeshaji wa reli ya kisasa - SGR, ikiwemo uendeshaji treni za umeme, ukarabati wa reli ya kisasa pamoja na kusimamia mifumo mipya ya mawasiliano na umeme katika Ukumbi wa Kambi ya SGR Ilala jijini Dar es Salaam hivi karibuni 2018.





Pichani; Matukio tofauti wakati wa ziara ya Katibu Mkuu wa Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano Dkt. Leonard Chamuriho alipotembelea Mradi wa Ujenzi wa Reli ya Kisasa – SGR, katika picha kushoto (wa tatu kushoto) akitazama kazi ya upimaji Mataruma ikiendelea katika Maabara Maalum ya kupima Mataruma iliyopo katika kambi ya SGR Soga mkoani Pwani, katika picha kulia ( wa kwanza kushoto) akipata maelezo kutoka kwa Meneja Mradi wa Ujenzi wa Reli ya Kisasa - SGR kipande cha Dar es Salaam hadi Morogoro Mhandisi Machibya Masanja (wa tatu kulia) kuhusu Maendeleo ya Ujenzi wa Reli ya Kisasa eneo la Kikongo Mkoani Pwani Desemba 2018.

TRC
# Reli na Matukio
Desemba 18, 2018 Toleo Namba 10.






Katika picha; Mkuu wa Wilaya ya Kisarawe Mhe. Jokate Mwegelo akipongezana na Mkurugenzi wa kampuni ya Yapi Merkezi inayojenga Reli ya Kisasa - SGR Bwana Fuat Kemal wakiwa pamoja na Katibu Tawala Wilaya ya Kisarawe Mtela Mwampamba (kulia) na Kaimu Meneja Uhusiano Shirika la Reli Tanzania Jamila Mbarouk (kushoto) baada ya kuweka jiwe la Msingi la Ujenzi wa Madarasa Matatu katika Shule ya Msingi Masanganya wilayani Kisarawe ikiwa ni sehemu ya Shughuli za kijamii kuunga mkono jitihada za Mkuu wa Wilaya ya Kisarawe katika Kampeni ya Tokomeza Ziro kwa kusaidia Ujenzi wa Madarasa matatu yaliaohidiwa na Mkurugenzi Mkuu wa TRC Ndugu Masanja Kungu Kadogosa wakati wa ufunguzi wa Harambee ya kampeni ya Tokomeza Ziro Kisarawe Desemba 2018.





Picha Kushoto; Meneja Mradi wa Ujenzi wa Reli ya kisasa - SGR kipande cha Dar - Morogoro Mhandisi Machibya Masanja akiwaelezea wakuu wa Mikoa Tanzania kuhusu hatua za uzalishaji Mataruma katika kiwanda cha Mataruma kilichopo kambi ya SGR Soga Kibaha, picha kushoto; Meneja Mradi wa Ujenzi wa SGR Mhandisi Machibya Masanja akiwaelezea wakuu wa Mikoa Tanzania kuhusu ubora wa reli pamoja na hatua za uwekaji wa reli walipofanya ziara kwa kutumia usafiri wa treni ya Deluxe kukagua Maendeleo ya Ujenzi wa Reli ya Kisasa Soga mkoani Pwani kuadhimisha Miaka 57 ya Uhuru wa Tanzania Bara kudumisha dhana ya tulikotoka, tulipo na tuendako Desemba 09 2018.



Meneja Mradi wa Ujenzi wa Reli ya Kisasa Dar es Salaam - Morogoro Mhandisi Machibya Masanja akiwaelezea wajumbe wa Kamati ya Bunge ya Maendeleo Endelevu kuhusu maendeleo ya Mradi walipofanya ziara ya siku mbili katika kambi za SGR za Ilala, Soga, Ngerengere na Kilosa kukagua maendeleo ya Mradi wa Ujenzi wa Reli ya Kisasa mapema mwezi Desemba 2018.



Wajumbe wa Kamati ya Bunge ya Maendeleo Endelevu wakitazama reli na Mataruma katika kambi ya Soga mkoani Pwani kabla ya kutembelea kiwanda cha Mataruma katika kambi ya Soga Kibaha mkoani Pwani walipofanya ziara kukagua maendeleo ya Mradi wa Ujenzi wa Reli ya Kisasa - SGR mapema mwezi Desemba 2018.